HOTUBA YA MGENI RASMI MOHAMMED KHAMIS ABDULLA KATIBU MKUU WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI WAKATI WA HAFLA YA KUTOA VYETI KWA WATAALAMU 30 WA TEHAMA WALIOPATA UFADHILI KUSHIRIKI MAFUNZO YA UZAMILI KWENYE MASOMO YA TEHAMA YENYE UHABA MCHACHE KWENYE VYUO MBALIMBALI NJE YA NCHI TAREHE 12/07/2024 UKUMBI WA MIKUTANO WA TAKWIMU

1. ***Bw. Juma Selemani Mkomi,*** Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,
2. ***Bi Justina Kaijage,*** Mwakilishi wa Benki ya Dunia,
3. ***Bi. Salome Kessy,*** Mkurugenzi wa Utawala na Uendelezaji wa Rasilimali Watu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Mwenyekiti wa Kamati ya Usimamizi wa Mafunzo kwa wataalamu wa TEHAMA kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali,
4. ***Bw. Mohamed Mashaka,*** Mkurugenzi wa Uendelezaji wa Mifumo na Huduma za TEHAMA, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari,
5. ***Bw. Bakari Mwamgugu,*** mratibu wa Mradi wa Tanzania ya Kidijitali,
6. ***Wajumbe wa Kamati*** ya usimamizi wa mafunzo ya wataalamu wa TEHAMA kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali.
7. ***Menejimenti na Watumishi*** mliopo kutoka Wizara ya Habari, Mawasiliano, na Teknolojia ya Habari,
8. ***Mwakilishi wa Benki ya CRDB,*** *Ofisi za Dodoma*

9. ***Wanufaika wa ufadhili wa mafunzo ya shahada ya Pili*** kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali;
10. ***Watumishi wenzangu,***
11. ***Waandishi wa Habari,***

Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana hapa siku hii ya Leo.

Pia napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu Mkuu Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa namna ambavyo umeendelea kusimamia kikamilifu utekelezaji wa mradi huu ambao unatekelezwa na Wizara tunazozisimamia. Lakini pia, tukio hili la leo linalenga mafunzo kwa watumishi ambapo masuala yote yanayohusu ustawi wa Watumishi yanasimamiwa na Wizara yako. **Tunakushukuru sana kwa Uwepo wako.**

Watumishi Wenzangu

Pia, nitumie nafasi hii kuipongeza Kamati ya usimamizi wa mafunzo kupitia mradi wa Tanzania ya Kidijitali inayoongozwa na Bi Salome Kessy kwa kazi nzuri iliyoifanya ya uhakiki na uchambuzi wa maombi 365 kwa weledi na kuzingatia taratibu zote na kuweza kupata watumishi 30 wanaotoka katika

Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali. Watumishi hawa 30 watakwenda kusoma nje ya nchi kwenye fani zinazohusiana na masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano zinazoibukia kama vile masuala ya Akili Bandia, Roboti, usalama wa mifumo ya mawasiliano na kadhalika.

Watumishi Wenzangu

Hafla ya leo inafanya idadi ya wanufaika kufikia 50 ambao wamepatiwa ufadhili katika shahada ya Uzamili katika maeneo mbalimbali nje ya nchi kama vile Uingereza - UK (42), Ujerumani (1), U.S.A (1), Malaysia (3), Uturuki (1), Sweden (1) na India (1) na ufadhili huu unatolewa kupitia mradi wa Tanzania ya Kiditali. Hili ni jambo kubwa na la kimkakati kwa Nchi yetu ambapo kwa sasa TEHAMA ni nyenzo muhimu na wezeshi katika kuchochea ukuaji wa uchumi wa Kidijiti. Kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania naishukuru Benki ya Dunia kwa kuwezesha ufadhili huu nje ya nchi kwa watumishi wa Serikali.

Watumishi Wenzangu

Napenda kutumia hadhara ya leo kufahamisha kuwa, zoezi la ufadhili wa mafunzo kwa wataalamu wetu wa TEHAMA linatoa taswira ya dhamira nzima ya jukumu la Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari katika kukuza uwezo na ubunifu wa Wataalamu wa TEHAMA nchini.

Kama ilivyoelezwa na Mwenyekiti wa Kamati ya usimamizi wa mafunzo ya wataalamu wa TEHAMA, kupitia mradi wa Tanzania ya Kidijitali jumla ya watumishi wa Serikali 500 watanufaika na programu hii ya kushiriki mafunzo ya muda mrefu na mfupi hii ni hatua kubwa na muhimu kwa nchi yetu.

Watumishi Wenzangu

Kama lilivyojukumu la Wizara kuwezesha mabadiliko ya teknolojia, ufadhili huu ni wa kimkakati na tunatarajia kuwa, vijana waliochaguliwa watatumia fursa hii kujifunza, kushirikiana na wenzao walio ng'ambo na hivyo kuboresha weledi na maarifa katika utendaji kazi wao baada ya kuhitimu mafunzo yao ili kulifaidisha Taifa kwa ujumla.

Hivyo, ninatoa rai kuwa maarifa na ujuzi mtakaopata utasaidia kuunda sio tu taaluma zenu bali kuwa mabalozi kwa watumishi wenzenu kwa mustakabali mzima wa kubuni, kuelimisha na kusukuma gurudumu la mabadiliko ya kidijitali nchini.

Watumishi Wenzangu

Moja ya vipaumbele vya Serikali ya awamu ya Sita kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ni kukuza vipaji na kukuza maendeleo ya wataalamu wa TEHAMA. Kufanikisha hili, juhudi mbalimbali zinafanyika ikiwa ni pamoja na kuweka Mazingira mazuri ya kisera, sheria na miundombinu. Masuala muhimu yanayoendelea kutekelezwa ni pamoja na:

a) Kukamilika kwa mkakati wa miaka 10 wa uchumi wa kidijitali ambapo pamoja na masuala mengine, mkakati umelenga ujenzi wa jamii ya kidijitali 'digital savvy society' itakayokuwa na weledi wa teknolojia za kidijitali.
b) Maboresho ya Sera ya TEHAMA yanayoendelea yatatilia mkazo kuendelea kukuza rasilimali watu ya wataalmu wa TEHAMA kupitia program muhimu na endelevu za kujenga ustadi, vipaji, weledi na maarifa ili kuwa washiriki hai katika ajenda ya mabadiliko ya kidijitali.
c) Kuunda Sheria ya Taifa ya TEHAMA, mipango ya kuimarisha na kusimamia ujuzi wa wataalamu utawekwa.
d) Kufanya ujenzi wa vyuo mahiri viwili (2) vya Teknolojia Dodoma na Kigoma ambavyo vitatoa program za mafunzo (demand based programs) kwenye eneo la Teknolojia mpya na zinazoibukia. Vyuo hivi vitakuwa ni miundombinu (state of art infrastructure) kwa wataalamu wa TEHAMA, wabunifu na Sekta za uzalishaji kukuza matumizi ya Teknolojia

mpya, kuwezesha uundaji wa Kampuni za TEHAMA, kufanya tafiti na ubunifu wa TEHAMA inayoendana na mipango mbalimbali ya maendeleo.

e) Kuwezesha ujenzi wa vituo nane (8) vya ubunifu kwenye maeneo ya Zanzibar, Arusha, Dodoma, Tanga, Kilimanjaro, Morogoro, Mbeya, Iringa, Mtwara, Mwanza na Dar-es-Salaam. Vituo hivi vitatumika kama miundombinu ya kuwawezesha vijana kuendeleza bunifu na tafiti zao katika TEHAMA ikiwemo matumizi ya teknolojia zinazoibukia kama vile Akili Bandia na Robotics.

Watumishi Wenzangu

Ni matumaini yangu kuwa, kupitia juhudi hizi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, itakuwa ni chachu pia kwa sekta binafsi kuendelea kuungana na Serikali kufanya uwekezaji wa kukuza rasilimali ya Wanatehama nchini. Kwa lengo la kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha TEHAMA kwa kuwa na wataalamu na wabunifu wabobevu Kitaifa na Kimataifa. Nashukuru uwepo wa Benki ya CRDB na kuonyesha kutuunga mkono kwenye juhudi hizi.

Watumishi Wenzangu

Naomba nimalizie kwa kunukuu maneno ya Bw. Mario Andretti Mmarekani aliyefanikiwa katika mashindano ya mbio za magari ya kasi duniani kuwa:

"Circumstances may cause interruptions and delays, but never lose sight of your goal. Prepare yourself in every way you can by increasing your knowledge and adding to your experience, so that you can make the most of opportunity when it occurs."

Nafahamu kuwa mnaenda kuanza maisha mapya ya masomo ughaibuni na ndio maana leo hii, Wizara ya Mambo ya Nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki imeweza kuwapa ufahamu na taratibu za namna ya kuishi vyema ughaibuni. Pamoja na changamoto zote mtakazozipata nawasihi mtumie fursa hii kutekeleza malengo ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mtambue kuwa "Chanzo pekee cha mafanikio ni ujuzi na uzoefu." Hivyo mkasome kwa bidii na kupeperusha bendera ya Taifa kwa uzalendo mkubwa na kwa kulinda maslahi ya Taifa.

Watumishi Wenzangu

Naomba niwatakie kila la Kheri na muwe na mafanikio kwenye safari yenu ya masomo.

Asanteni sana.